**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU BUSTANI**

Simu Nambari**: 255-26-2360033**
E-MailNo**.** **bustanitc@gmail.com**

**Mobile No. 0692063663**
**0758045763**
**0743133331**

Chuo cha Ualimu Bustani,
S.L.P. 131,
**KONDOA.**

11/06/2026

**NDG: …………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA STASHAHADA YA ELIMU MSINGI MCHEPUO WA SAYANSI YA JAMII KWA LUGHA YA KISWAHILI,**
**MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

**1. UTANGULIZI:**

Ninayo furaha kukuarifu rasmi kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada ya Ualimu katika Chuo Cha Ualimu Bustani. Chuo kina dhamira ya kuwa kituo cha kuibua na kuendeleza stadi za Ualimu kwa kujikita katika maeneo ya Sayansi na Technolojia, Sayansi ya jamii (social Science) katika masomo ya Historia ya Tanzania na maadli ,Jiografia na mazingira ,masomo ya Ualimu, ujasiliamali na stadi za maisha ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji nchini. Hivyo unapaswa kuthamini uchaguzi huu kwa kusoma kwa bidii, kufuata taratibu na kanuni za Chuo ili uweze kufikia malengo yako binafsi na malengo ya Taifa kwa ujumla.

**2. MAHALI CHUO KILIPO**

Chuo cha Ualimu **Bustani** kipo Mkoa wa **Dodoma,** Wilaya ya **Kondoa**. Kipo kilometa 3.5 kutoka standi kuu ya magari (**Bicha**) au kilometa 2 kutoka stendi ya mabasi Kondoa mjini

**3. KOZI ZINAZOFUNDISHWA CHUONI**

Chuo cha ualimu Bustani kinafundisha kozi zifuatazo:

i. Stashahada ya ualimu Elimu msingi sayansi ya jamiii kwa miaka miwili (2)
ii. Stashahada ya ualimu Elimu msingi sayansi jamii kwa walimu kazini kwa njia ya masafa miaka mitatu (3)

4. **TAREHE YA KURIPOTI CHUONI KWA WANACHUO WOTE:**

Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe 17/08/2026 na tarehe ya mwisho kuripoti ni tarehe 01/09/2026 bila kukosa ili kuanza mafunzo. Iwapo hutafika chuoni mpaka tarehe 01/09/2026 hutapokelewa. Mara baada ya kuwasili Chuoni fika ofisi ya usajili ambapo utapokelewa na kupewa maelekezo. Mwanachuo haruhusiwi kwenda bwenini au maeneo mengine ya chuo kabla ya kusajiliwa. Ili uweze kusajiliwa unatakiwa uwe na vitu vifuatavyo:

- Fomu ya maelekezo ya kujiunga na Chuo (Joining instruction).
- Cheti halisi cha matokeo ya kidato cha nne na nakala yake.
- Cheti halisi cha matokeo ya kidato cha sita na nakala yake.
- Hati ya matokeo ya kidato cha sita (Result slip) kwa wale waliohitimu kidato cha sita Mei 2025 (na nakala zake)
- Cheti halisi cha Ualimu ngazi ya Astashahada (Daraja la tatu A) na nakala yake.
- Cheti halisi cha kuzaliwa na nakala yake.
- Cheti cha kumaliza kidato cha sita (Leaving certificate)
- Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA.
- Risiti za malipo ya michango (Original bank pay in-slip)
- Bahasha (A4) na nakala za vyeti

**N.B Hautapokelewa wala kusajiliwa usiporipoti na mahitaji haya**

5. **VIFAA VINAVYOHITAJI KAKUJA NAVYO KWA WANACHUOWA STASHAHADA YA MIAKA MIWILI**

**a. Vifaa vya malazi**

Mashuka mawili rangi ya blue bahari, blanketi 1, mto 1, chandarua nyeupe 1 na foronya 2 za blue bahari.

**b. Vifaa vya chakula**

Vyombo vya kulia chakula (sahani 1, kikombe 1, bakuli 1, kijiko 1) galoni ya lita tano ya plastiki kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa yaliyochemshwa, pamoja na ndoo moja ya lita kumi kwa ajili ya kuogea

**c. Vifaa vya michezo**

Nguo za michezo (bukta na T-shirt rangi yoyote pamoja na raba jozi moja ya rangi yoyote, track suti rangi ya **Blue bahari** kwa ajili ya mchakamchaka na jogging siku za Jumamosi na ziara za kimichezo.

**d.Vifaa vya taaluma.**

- Daftari zisizopungua **15 QUIRE 3**, kalamu za wino, mkebe wa Hisabati.
- Unatakiwa kuja na muhtasari wa masomo ya shule za msingi na kozi uliyochaguliwa.
- Karatasi **Rimu 1 (A4)**

e . **vifaa vya shughuli za bustani na usafi wa mazingira ya chuo.**

- **Unatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo; Jembe-kila mwanachuo, Reki – wavulana tu, Fagio ndefu za chelewa (chelewa kubwa) – wasichana tu.**

6. **VIFAA VINAVYOHITAJI KWA WANACHUO WA STASHAHADA YA MIAKA MITATU WALIMU KAZINI ( MASAFA)**

- Daftari zisizopungua **15 QUIRE 3**, kalamu za wino, mkebe wa Hisabati.
- Unatakiwa uwe na muhtasari wa masomo ya shule za msingi za kozi uliyochaguliwa.
- Kuwasilisha karatasi **Rimu 1 (A4**) kwa ajili ya kazi za kitaaluma.

7. **ADA YA CHUO KWA WANACHUO WOTE STASHAHADA MIAKA MIWILI NA MITATU.**

Ada ya mafunzo ni **Tsh 450,000/=** kwa mwaka, au unatakiwa kulipa kiasi kisichopungua **Tsh 225,000/= kwa** muhula. Fedha hiyo unapaswa kuingiza kwenye simu ya mtandao wowote na utapata maelekezo ya namna ya kulipa ada kwa kutumia **control** number ukifika Chuoni. Kwa wanachuo wa Stashahada ya ualimu miaka mitatu walimu kazini( Masafa) Mwanachuo atawasiliana na kuomba namba ya malipo ya ada ya chuo (control number)na kulipa ada ya mafunzo serikalini.Mwanachuo hatasajiliwa asipolipa ada na michango.

8. **. MICHANGO YA CHUO KWA WANACHUO WA STASHAHADA YA MIAKA MIWILI**

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Ulinzi | 30,000/= kwa mwaka |
| 2 | Ukarabati | 25,000/= kwa mwaka |
| 3 | Usafi na Mazingira | 20,000 kwa mwaka |
| 4 | Huduma ya kwanza | 10,000/= kwa mwaka |
| 5 | Michezo | 30,000/= kwa mwaka |
| 6 | Kukodi godoro | 10,000/= kwa mwaka |
| 7 | Usajili | 20,000/= kwa mwaka |
| 8 | Mchango wa serikali ya wanachuo | 5,000/= kwa mwaka |
| 9 | Mchango wa bima ya afya **(NHIF)** | 50,400/= **kwa asiyekuwa nayo** |
| | **JUMLA KUU** | **200,400/=** |

Jumla ya michango ya Chuo Tsh **195,400**/= kwa mwaka ziwekwe kwenye account namba **50201100020 (NMB) (BUSTANI TEACHERS' COLLEGE FUND**) bila kukosa
Mchango wa serikali ya wanachuo **5,000/=** iwekwe kwenye account namba **50210010117 (NMB) (BUSTANI STUDENT ORGANISATION).**

9. **MICHANGO YA CHUO KWA STASHAHADA YA UALIMU KWA WALIMU KAZINI MIAKA MITATU (NJIA YA MASAFA)**


Michango ya chuo kwa wanachuo wa stashahada ya miaka mitatu kwa njia ya walimu kazini (Masafa) ni kama ilivyoorodheshwa:

i. Mchango wa usajili Tsh. 20,000/= kwa mwaka
ii. Mchango wa huduma ya kwanza Tsh.10,000/= kwa mwaka
iii. Mchango wa serikali ya wanachuo T sh.5000/= kwa mwaka
iv. Ufuatiliaji na uendeshaji wa mafunzo Tsh. 70,000/= kwa mwaka
v. Ukarabati T. sh. 25,000/= kwa mwaka
vi. Vifaa vya usafi Tsh .20,000/= kwa mwaka

**Jumla ya michango yote kwa mwaka ni Tsh. 150,000/= kwa mwaka. Fedha** ziwekwe kwenye account namba **50201100020 (NMB) (BUSTANI TEACHERS' COLLEGE FUND**) bila kukosa
Mchango wa serikali ya wanachuo **5,000/=** iwekwe kwenye account namba **50210010117 (NMB) (BUSTANI STUDENT ORGANISATION).**

**N.B.Jumla ya fedha za ada na michango kwa mwaka ni Tsh.600,000 tu.** Wasilisha risiti za malipo ya Bank kwa msajili ukifika Chuoni na risiti ya malipo ya ada. Aidha **usije** na fedha tasilimu chuoni.Fuata maelekezo kwa kila kipengele cha malipo unayofanya **Usichanganye** akaunti wala usilipe ada katika akaunti ya michango kuepuka usumbufu.


## 10. SARE ZA CHUO



**WANAUME**

i. Suruali ya buluu nyeusi (darkblue) na nyeusi zenye marinda mawili yenye mkunjo chini (turn up). Suruali nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na suruali ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na suruali linaweza kuvaliwa. Suruali itavaliwa na mkanda mweusi.
ii. Shati liwe buluu bahari (light blue) mikono mirefu.
iii . Tai ndefu buluu nyeusi (dark blue) au nyeusi. Tai itavaliwa kuendana na rangi ya suruali.
iv . Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza (kufunika) kisigino kifupi. Viatu vitavaliwa na soksi ndefu nyeusi.
v .Hairuhusiwi kuvalia suruali chini ya kiuno (mlegezo).

**WANAWAKE**



i. Sketi rinda boksi ya buluu nyeusi (dark blue) na nyeusi zenye
urefu unaozidi magoti na zisizobana. Sketi nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na sketi ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na rangi ya sketi linaweza kuvaliwa.
ii. Shati iwe ‘light blue’ mikono mirefu na tai ndefu ‘dark blue’ au nyeusi. Tai iendane na rangi ya sketi.
iii . Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza kisigino kifupi, na soksi ndefu nyeupe.
iv . Soksi nyeupe jozi mbili na zaidi
v .Sweta jeusi na koti linalofanana na rangi ya sketi kwa siku husika sketi.
vi . Nywele zibanwe au zisukwe mtindo wa utii wa roda (twende kilioni) mistari mitano (5) hadi nane (8) au kubanwa kisogoni kwa kibanio cheusi kisicho na urembo wowote.
vii. Kwa wanachuo wa dini ya kiislamu wanajisitiri kwa Hijabu ,lazima iwe inaendana na rangi ya shati analovaa kwa siku husika.
viii .Hairuhusiwi kuvaa nguo,angavu zenye kuonesha maumbile.
Ix. Kwa wanachuo wa dini ya kiislamu wanajisitiri kwa Hijabu, lazima rangi iendane na ya shati analovaa kwa siku husika.

**MUHIMU:**

i. Ilikupata mfanano wa sare za chuo na zinazokubalika unashauriwa kupata maelekezo ya kina kutoka chuoni kabla ya kushona au kununua

ii. Kila mwanachuo anapaswa kuwa na T-Shirt ya blue bahari yenye nembo ya chuo inayopatikana chuoni kwa gharama ya Tsh 20,000/=. Fedha hiyo iwekwe kwenye akauti namba **50210010117 (NMB) (BUSTANI STUDENT ORGANISATION).**

iii. Kila mwanachuo atatakiwa kuchangia gharama ya mahafali kiasi cha Tsh10,000/= kwa mwaka

iv. Fedha hiyo iwekwe kwenye akauti namba **50201100020 (NMB) (BUSTANI TEACHERS' COLLEGE FUND**)

**MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA YA WANACHUO**

i. Mwanachuo anashauriwa aje na fedha tasilimu kwa ajili ya matumizi binafsi.
ii. Mwanachuo mwenye kadi ya bima ya afya ni muhimu kuja nayo.
iii. Mwanachuo atapaswa kufanya uchunguzi wa afya katika Hospitali za wilaya au mikoa kwa kutumia fomu iliyoambatanishwa hapo chini.

**11. CHAKULA**

i. Chuo kinatoa chakula kwa mujibu wa miongozo ya serikali.
ii. Chuo hakitoi chakula maalum (**special diet**) kwa wanachuo wenye mahitaji hayo

**12. SHUGHULI ZA UZALISHAJI MALI CHUONI**


Ili kutekeleza mtaala wa mafunzo ya **Elimu ya Ualimu** kwa ufanisi chuo kinaendesha shughuli za kilimo hususani bustani za mboga mboga, mahindi ya umwagiliaji na migomba . Lengo kuu ni kuwafanya wanachuo wajifunze kwa nadharia na vitendo katika masomo yao hususani stadi za maisha, ili kutekeleza mtaala wa **Ualimu ambao unazingatia falsafa ya elimu ya kujitegemea unatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo; Jembe-kila mwanachuo, Reki – wavulana tu, Fagio ndefu za chelewa (chelewa kubwa) – wasichana tu.**

**13. MWISHO**


Jumuiya ya chuo cha Ualimu Bustani inakutakia maandalizi mema ya safari ya kuja chuoni.

**KARIBU SANA**

Asante



SABINA GADIYE TSOAY
KAIMU MKUU WA CHUO




**NAKALA:**

i. Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S. L. P 10,
**DODOMA.**

ii. Mkurugenzi Mafunzo ya Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S. L. P 10`,
**DODOMA.**

iii. Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule,
Kanda ya Kati,
**DODOMA**

(iv) Afisa Elimu (M),
**DODOMA**

(v) Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo,
Chuo cha Ualimu Bustan

**KANUNI ZA WANACHUO**

UTANGULIZI

Miongozo na taratibu za mafunzo ya ualimu zinalenga kuwaandaa walimu wenye mtazamo, tabia na uelekeo wa taaluma ya ualimu. Mtazamo, tabia na uelekeo mzuri hujengwa na kukuzwa kutokana na matendo mema, amabyo huakisi utii wa kanuni ,sheri, taratibu na miogozo . Kanuni na taratibu zifuatazo zitawezesha uendeshaji na usimamizi wa mafunzo ya ualimu kwa wanachuo kwa kiwango cha juu cha ufanisi na ubora kwa walimu tarajali na walimu kazini.

**1. UTII WA SHERIA ZA NCHI NA ALAMA ZA TAIFA**

i. Mwanachuo atawajibika kutii na kuzifuata Sheria za nchi.

ii. Mwanachuo atawajibika kuzitii Alama za Taifa kama vile Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa na Wimbo wa Taifa.

**iii.** Mwanachuo hataruhusiwa kwa namna yoyote ile katika mazingira yoyote yale kufanya udanganyifu ikiwa ni pamoja na kughushi nyaraka za kiserikali, kielimu au kiofisi.

❖ **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni sambamba na kuchukuliwa hatua kwa utaratibu uliowekwa na Sheria za nchi, atastahili adhabu ya papo kwa papo ambayo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/ kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa makosa kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

2. HESHIMA NA UTII

i. Mwanachuo ajiheshimu mwenyewe, awaheshimu wenzake, wafanyakazi na watu wengine anaokutana nao. Salamu itolewe kwa heshima kwa kuzingatia utamaduni na maadili ya Kitanzania.

ii. Mwanachuo awe na lugha yenye hadhi ya taaluma ya ualimu na matendo yake yawe yanakuza heshima na utu wake. Aidha, lugha zinazoruhusiwa kwa mawasiliano hapa chuoni ni Kiswahili na Kiingereza.

iii. Mwanachuo anapaswa kuheshimu na kufuata ratiba ya Chuo na shughuli zinazoambatana na ratiba.

iv. Mwanachuo anapaswa kuwa mtiifu kwa kengele au ishara nyingine yoyote itakayomhitaji kufika mahali anapotakiwa.

v. Mwanachuo sharti awahi wakati wote anapohitajika chuoni mfano: kuripoti chuoni, mstarini, bwaloni, ukumbini, darasani, katika kazi za nje na mahali pengine.

vi. Mwanachuo haruhusiwi kujihamisha bweni au chumba alichopangiwa. Aidha kwa namna yoyote ile mwanachuo haruhusiwi kulala bweni ambalo hakupangiwa.

vii. Mwanachuo haruhusiwi kufanya udanganyifu na au upotoshaji wa taarifa wa aina yoyote kwa jambo lolote wakati wote wa mafunzo.

❖ **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atafunguliwa mashtaka na kupewa adhabu ya papo kwa papo na kiongozi wa serikali ya wanachuo, mkufunzi au Mratibu wa masuala ya wanachuo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo kabisa.**

❖ **3.MAHUSIANO**

i. Mwanachuo wa kike haruhusiwi kwenda bweni la wanaume na mwanachuo wa kiume haruhusiwi kwenda bweni la wanawake bila idhini maalum kutoka ofisi ya uratibu wa masuala ya wanachuo.
ii. Mahusiano kati ya wanachuo, walezi na jamii yanapaswa kuwa ya kuheshimiana. Wanachuo walio kwenye ndoa watoe uthibitisho wa cheti cha ndoa kwa Mratibu wa masuala ya wanachuo na wafuate kanuni na taratibu za Chuo.
iii. Mahusiano ya kingono na mtu yeyote hayaruhusiwi.
iv. Mwanachuo anaruhusiwa kutembelewa au kupokea mgeni siku za mwisho wa wiki au sikukuu na sio siku za masomo. Mwanachuo anaelekezwa kuongea na mgeni wake katika maeneo yatakayoruhusiwa na Chuo. Wageni wanaruhusiwa kuingia chuoni kuanzia saa 5:00 asubuhi na kuondoka chuoni kabla ya saa 11.00 jioni.
v. Mgeni wa dharura wa mwanachuo (atakayekuja chuoni siku za masomo) aelekezwe kuonana na Mratibu wa masuala ya wanachuo.
vi. Mgeni wa mwanachuo haruhusiwi kutembelea au kupumzika katika mazingira ya Chuo pasipo ruhusa ya Uongozi wa Chuo.
vii. Mwanachuo haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mtumishi yeyote bila ruhusa maalumu kutoka kwa Mratibu wa Masula ya Wanachuo.

**Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo kabisa.**

**4. USAFI, AFYA NA MAZINGIRA** :

i. Mwanachuo anatakiwa kuwa na nywele fupi zisizozidi urefu wa sentimeta moja (sm 1) na zinazotunzwa vizuri kwa kuoshwa na kuchanwa. Aidha, wasichana watakaopenda kusuka nywele wanaelekezwa kusuka mtindo wa utii wa roda (twende kilioni) kuanzia mistari mitano (5) hadi nane (8). Kwa watakao bana nywele wanaelekezwa kubana kisogoni kwa kibanio cheusi. Aidha, mwanachuo haruhusiwi kuweka dawa nywele, rasta (dreads), au kubadili nywele rangi (bleaching).
ii. Mwanachuo anapaswa kuoga kila siku na kuonekana safi wakati wote
iii. Mwanachuo haruhusiwi kuwa na kucha ndefu, ndevu na meno yasiyopigwa mswaki.
iv. Mwanachuo haruhusiwi kupaka rangi za kucha, midomo na kutinda nyusi au kuweka nyusi bandia au kucha bandia.
v. Mavazi ya mwanachuo sharti yawe safi na heshima wakati wote.
vi. Mwanachuo anawajibu wa kuweka matandiko yake na vitu vingine chumbani katika hali ya usafi na unadhifu.
vii. Mwanachuo anawajibika kufanya usafi wa maeneo, bweni, bwalo la chakula, madarasa, kumbi, vyoo pamoja na maeneo mengine nyakati za asubuhi na siku za mpango kazi. Mwanachuo ambaye hatashiriki usafi atahesabika kuwa ni mtovu wa nidhamu.
viii. Mwanachuo haruhusiwi kujihusisha na: Matumizi ya vileo na madawa ya kulevya, uvutaji wa sigara au bangi, matumizi ya ugolo au kubeli, vitendo vya ushoga, ubakaji au usagaji, wizi, utapeli, unyang'anyi au kamari ya aina yoyote.
ix. Wagonjwa wanaelekezwa kwenda zahanati/hospitali kupata ushauri na matibabu. Ruhusa za mapumziko bwenini zitatolewa na mganga, muuguzi, Mratibu wa masuala ya wanachuo au mkufunzi wa zamu.

x. Mwanachuo atakayebainika kuwa ana ujauzito atashauriwa kwenda nyumbani kwa sababu za kiafya na miezi sita baada ya kujifungua mwanachuo anaweza kuomba kurejea chuoni kwa kuandika barua kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia kwa Mkuu wa Chuo.

xi. Mwanachuo atakayebainika kutoa au kujaribu kutoa mimba atakuwa amefanya kosa kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za nchi, hivyo atawajibishwa.

**Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo kabisa**.

**5. MAVAZI:**

i. Mavazi yatakayovaliwa na mwanachuo wakati wote Chuoni sharti yawe ya heshima, safi na yenye kuendana na masharti kwenye kanuni hizi.

ii. Mwanachuo analazimika kuvaa sare kamili ya Chuo wakati wote na mahali popote (ndani na nje ya chuo) katika kipindi chote cha masomo (semista/muhula) ; isipokuwa wakati wa kazi za nje, nyakati za jioni baada ya masomo, au siku za mapumziko ndani ya chuo.

iii. Mwanachuo anatakiwa kuvaa kitambulisho chake shingoni wakati wote awapo chuoni au nje ya chuo kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma.

**1. SARE KWA WANAUME**

i. Suruali ya buluu nyeusi (darkblue) na nyeusi zenye marinda mawili yenye mkunjo chini (turn up). Suruali nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na suruali ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na suruali linaweza kuvaliwa. Suruali itavaliwa na mkanda mweusi.

ii. Shati liwe buluu bahari (light blue) mikono mirefu.

iii. Tai ndefu buluu nyeusi (dark blue) au nyeusi. Tai itavaliwa kuendana na rangi ya suruali.

iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza (kufunika) kisigino kifupi. Viatu vitavaliwa na soksi ndefu nyeusi.

v. Hairuhusiwi kuvalia suruali chini ya kiuno (mlegezo).

vi. Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe na ‘track suit’ ya buluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe wakati wa michezo tu.

vii. Uvaaji wa jinzi, kaptula, bangili, cheni, vimodo, skafu, makobazi, na pete (zisizo za ndoa) na vingine vinavyofanana na hivyo hauruhusiwi.

**Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo kabisa.**

**2. SARE KWA WANAWAKE**

i. Sketi rinda boksi ya buluu nyeusi (dark blue) na nyeusi zenye urefu unaozidi magoti na zisizobana. Sketi nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na sketi ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na rangi ya sketi linaweza kuvaliwa.

ii. Shati iwe ‘light blue’ mikono mirefu na tai ndefu ‘dark blue’ au nyeusi. Tai iendane na rangi ya sketi.

iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza kisigino kifupi, na soksi ndefu nyeupe.

iv. Nywele zichanwe au zisukwe mtindo wa utii wa roda (twende kilioni) mistari mitano (5) hadi nane (8) au kubanwa kisogoni kwa kibanio cheusi.
v. Mwanachuo atakayependa kujisitiri kwa vazi la hijab anaelekezwa kumwona mlezi wake wa kike chuoni au Mkuu wa Chuo kwa maelekezo bayana.
vi. Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe na 'track suit' ya buluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.
vii. Uvaaji wa nguo angavu, khanga, kitenge, kofia, kilemba, hereni, bangili, mkufu, shanga, pensi, sketi fupi, nguo zenye mpasuo unaozidi magoti, makobazi na pete (isipokuwa pete ya ndoa) hauruhusiwi.
viii. Uvaaji wa mavazi yasiyokubalika katika kanuni
ix. utapelekea mavazi hayo kuchukuliwa na kuhifadhiwa ofisi ya Mratibu wa masuala ya wanachuo na kufuatiwa na adhabu ya papo kwa papo. Mavazi yaliyoshikiliwa yatarejeshwa kwa mwanachuo atakapomaliza mafunzo.

❖ **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo**.

**7. RUHUSA:**

i. Mwanachuo atakayetaka kutoka nje ya mipaka ya Chuo kwa shughuli binafsi au za ofisi, atapaswa kujaza fomu ya ruhusa kutoka kwa Mkufunzi wa zamu isipokuwa siku itakapotolewa ruhusa ya jumla.
ii. Ruhusa zitakazopelekea mwanachuo kulala nje ya chuo zitatolewa na Mkuu wa Chuo kupitia Ofisi ya Masuala ya Wanachuo.
iii. Mwanachuo anaelekezwa kutoa taarifa kwa kiongozi wa bweni au mkufunzi wa bweni au Mratibu wa masuala ya wanachuo juu ya mwanachuo mwenzake ambaye hayupo Chuoni au hakulala bwenini bila ruhusa kutoka kwa Mkuu wa Chuo.
iv. Muda wa mwisho wa mwanachuo kumtembelea mwanachuo mwenzake bwenini wakati wa usiku ni saa nne usiku.
v. Ruhusa ya jumla kwa wanachuo itatolewa siku ya Jumamosi na Jumapili pamoja na siku za Sikukuu kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni wakiwa wamevaa sare za Chuo. Aidha, ruhusa itatolewa kwa waamini wa dini ya kiislam siku ya Ijumaa kati ya saa 6:00 mchana mpaka saa 8:00 Alasiri.
vi. Siku za Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu ambapo hutolewa ruhusa ya jumla kwa wanachuo kutoka nje ya Chuo, kutakuwa na 'roll call' saa 11:30 jioni ambayo kila mwanachuo lazima ahudhurie. Aidha 'roll call' inaweza kuitishwa wakati wowote itakapoonekana inafaa.
vii. Mwanachuo anapotoka chuoni atumie njia zilizo rasmi za usafiri kama vile kufuata barabara au usafiri wa umma.
viii. Mwanachuo hataruhusiwa kutembelea klabu za pombe, kumbi za starehe na nyumba za kulala wageni, nyumba/majengo ya michezo ya kamali na michezo ya kubashiri wakati wa mafunzo.

❖ **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro,**

**kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo**.

**8.TAALUMA**

i. Mwanachuo anapaswa kuheshimu na kufuata ratiba ya Chuo itakayoanza saa 11:30 asubuhi na kumalizika saa 4:00 usiku.
ii. Mwanachuo anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani na vipindi vya muda wa ziada.
iii. Mwanachuo anawajibika kuwahi na kukaa darasani muda wote wa masomo.
iv. Iwapo mwanachuo atakuwa hana kipindi kwa mujibu wa ratiba ya masomo atapaswa kuwa darasani, maktaba au chumba cha TEHAMA au eneo lingine kwa ruhusa maalumu.
v. Mwanachuo anatakiwa kushiriki kikamilifu na kuonesha jitihada katika masomo yote yanayotolewa katika kozi anayosoma, kuhudhuria darasani, kufanya majaribio na mitihani yote.

**Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo**.

**9. CHAKULA :**

i. Huduma ya chakula itatolewa kwa Mwanachuo aliyesajiliwa na kufuata utaratibu wa utoaji wa chakula.
ii. Milo yote lazima iliwe kwenye Bwalo la chakula isipokuwa kwa kibali maalum. Mwanachuo haruhusiwi kupeleka chakula Bwenini.
iii. Mwanachuo haruhusiwi kupika au kuwa na Vifaa kama jiko, ‘heater’, sufuria na kisu Bwenini au mahali pengine popote.
iv. Mwanachuo haruhusiwi kumkaribisha mtu yeyote kula chakula cha Chuo bila kupewa kibali maalum na Mkuu wa Chuo au mtu anayehusika.
v. Mwanachuo haruhusiwi kuingia bwaloni na viatu vya wazi (makobazi), kandambili, kaptula, kanga, vesti, gauni ya kulalia, skafu, taulo, kofia, na vitu vinavyo fanana na hivyo.

❖ **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

**10 .UTUNZAJI WA MALI ZA CHUO :**

i. Mwanachuo anaelekezwa kutumia mali ya Umma vizuri kama umeme na maji ili kuimarisha uendelevu na kuepuka gharama zisizo za lazima.
ii. Kiongozi wa bweni na wanabweni wana wajibu wa kutunza mali zote za bweni na nyaraka muhimu.
iii. Mwanachuo haruhusiwi kufanya marekebisho au maunganisho ya mtandao, umeme au maji pasipo ruhusa maalum.
iv. Mwanachuo haruhusiwi kuandika, kuchora au kupaka rangi katika majengo au vifaa mbali mbali pasipo maelekezo maalumu.

v. Mwanachuo anaelekezwa kurejesha kwa wakati mali ya Umma iliyoazimwa.
vi. Wizi wa mali ya umma au mali ya mtu mwingine ni kosa la kinidhamu kwa mujibu wa kanuni hizi na jinai kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi.
vii. Milango ya majengo na mabomba za maji yafungwe na Taa zizimwe wakati ambapo havitumiki. Viongozi wa mabweni watawajibishwa kwa kutokutekeleza kanuni hii.
viii. Mwanachuo haruhusiwi kujihusisha na biashara yoyote chuoni.

- **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni anaweza kupewa adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua), kulipa gharama yote ya uharibifu alioufanya au kusababisha au adhabu nyingine inayofanana na hizo. Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

**11.HABARI NA MAWASILIANO :**

i. Mawasiliano yafanyike kwa kuzingatia daraja/hadhi ya mtu mfano : kiongozi,mkufunzi,wafanyakazi wasio wakufunzi, n.k. Lugha ya matusi, kejeli, dharau, dhihaka na lugha za kudhalilisha hazitavumiliwa.
ii. Mawasiliano yote rasmi nje ya Chuo ni lazima yafanywe kupitia ofisi ya Mkuu wa Chuo. Hii ni pamoja na mialiko ya michezo, mikutano, semina, warsha baina ya wanachuo na watu au jumuiya ya nje.
iii. Taarifa ya msiba, ugonjwa na taarifa nyingine muhimu kutoka nyumbani zinazomuhusu mwanachuo ziwasilishwe Ofisi ya Mratibu wa Masuala ya Wanachuo na mtoa taarifa.
iv. Wanachuo hawaruhusiwi kukusanyika au kufanya mkutano bila idhini ya Mkuu wa Chuo.
v. Mwanachuo haruhusiwi kupiga kelele, kufungulia redio au chombo chochote cha muziki kwa sauti ya juu kiasi cha kuleta usumbufu kwa majirani zake.
vi. Mwanachuo au mtu yeyote yule haruhusiwi kupiga picha au kurekodi taarifa yeyote na kurusha katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii bila idhini ya mhusika au Mkuu wa Chuo.
vii. Matumizi yasiyo rasmi ya vifaa vya kielektroniki kama vile simu kwenye vyumba vya mitihani, darasani au kwenye mikusanyiko maalumu hayaruhusiwi bila idhini ya Mkuu wa Chuo.

- **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

**12. ULINZI NA USALAMA :**

i. Mwanachuo anatakiwa kutii tahadhari zote za ulinzi na usalama.
ii. Mwanachuo anatakiwa kutoa taarifa kwa uongozi wa Chuo mara tu kunapotokea viashiria vya hali au tukio lisilo la kawaida.
iii. Mwanachuo anawajibu wa kuwa mlinzi wa mali yake binafsi na mali ya umma.
iv. Mwanachuo haruhusiwi kushawishi, kuongoza, kushiriki mgomo na maandamano ya aina yeyote bila kibali.
v. Mwanachuo haruhusiwi kumiliki aina yoyote ya silaha chuoni.
vi. Mwanachuo hatakiwi kutoa matamshi yanayopelekea taharuki na au chuki na kuhatarisha usalama wake binafsi na au usalama wa wenzake/chuo.

- **Mwanachuo hatakiwi kugombana na au kuhatarisha usalama wake binafsi na au usalama wa wenzake/chuo. Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hii kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo**.

**KUWA MWALIMU BORA NA MWENYE MAADILI INAWEZEKANA**

**TIMIZA WAJIBU WAKO--KARIBU SANA .**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU BUSTANI**

Simu Nambari**: 255-26-2360033**
E-MailNo**.**
[bustanitc@gmail.com](mailto:bustanitc@gmail.com)

Mobile No**. 0692063663**
**075 045763**
**0743133331**

Chuo cha Ualimu Bustani,
S.L.P. 131,
**KONDOA.**

11/06/2027

Mimi ………………………………………………………………………………………………… Niliye chaguliwa kujiunga na CHUO CHA UALIMU BUSTANI mwaka 2026/2027 nimesoma maelekezo ya kujiunga na chuo pamoja na sheria na taratibu za Chuo hivyo ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yangu binafsi, Malengo ya Chuo na Taifa kwa ujumla.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu na nyeti kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika mafunzo yangu nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajila yangu pia. Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa chuoni:

1. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu kama Mwalimu tarajali
2. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za chuo kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazo tolewa mara kwa mara na uongozi wa Chuo
3. Sitajihusisha na vitendo vya utovu wa nidhamu katika muda wote wa mafunzo
4. Nitakubali kupewa huduma stahiki kama chakula kulingana na taratibu na mwongozo wa chakula unaotolewa na wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.
5. Nitashiriki katika shughuli zote za nje ya darasa kwa moyo wa kizalendo ili kukitumikia chuo na taifa langu.
6. Ikiwa nitakikiuka kiapo hiki pamoja na kanuni na taratibu za chuo kama nilivyozisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani na kumwita mzazi/mlezi wangu…………………………………………………………………………(Jina la Mzazi/Mlezi) kwa ajili ya hatua zaidi na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayotolewa na Kamati ya nidhamu ya Chuo kwa mujibu wa sharia kanuni na taratibu za chuo.

Saini ya Mwanafunzi…………………………………………Tarehe……… Mwezi …………Mwaka 2026

***SEHEMU YA MZAZI/MLEZI***

Mimi……………………………………………………………………………………………………….. ninakubali

kupokea nafasi yakijana wangu (jina)……………………………………………..kujiunga katika Chuo cha Ualimu Bustani mwaka wa masomo 2026/2027. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya chuo kwa wakati kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na chuo. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na Chuo kwa kulipa michango kwa wakati ili kumwezesha mwanangu kutekeleza wajibu wake kwa chuo na Taifa kwa ujumla

Anuani yangu ya kudumu, S.L.P……………………………………………………………………………...
Wilaya …………………………………………………………………………..
Mkoa ………………………………………………………….
Makazi…………………………………………………………………………….
Shughuli/kazi…………………………………………………………………………

Simu……………………………………………………………………………………….
Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nitajulisha Chuo kwa maandishi ili kurahisisha mawasiliano

Saini: Mzazi/Mlezi…………………………………..…………

Tarehe………Mwezi…… Mwaka 2026

## GOVERNMENT OF TANZANIA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO: The Medical Officer,

**PART A:**

Please examine
Mr/Mrs/Miss……………………………………………………………………………………..
To his/her physical and mental fitness for a full time a part time vocational course.

A: 1. (i) Eye – sight
(ii) Hearing
(iii) Speech
(iv) Venereal Diseases
(v) Leprosy
(vi) Limbs
(vii) Epilepsy

2. Neuroses
3. Other serious diseases. B: Blood Group

Date: ……………………. Signature………………Official Stamp……………………………

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above-named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a part time vocational course.

I. (a) Eye – sight……………………………………………………
(b) Hearing……………………………………………………...
(c) Limbs…………………………………………………………
(d) Speech……………………………………………………….
(e) Leprosy………………………………………………………
II. Neuroses………………………………………………………………
III. Other serious
(a) Diseases……………………………………………………..
(b) Pregnancy……………………………………………………

**Date: ……………………….. Signature………………… Official stamp.....................................**